MOSHI
TANZANIA

# MANISPAA YETU

www.moshimc.go.tz | Toleo La 02 | Kitengo cha Mawasiliano | Manispaa ya Moshi




HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI MUNICIPAL COUNCIL

moshimanispaa    www.moshimc.go.tz

**JANUARI - MACHI 2023**

HALIUZWI



**WANANCHI WA KATA YA MSARANGA WAMPONGEZA RAISMHE . DR . SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUWAJENGEA SHULE YA SEKONDARI .**

WANANCHI wa Kata ya Msaranga, Manispaa ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zilizofanikisha ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Msandaka kwenye Kata hiyo.

Pongezi hizo zimetolewa na Diwani wa Kata ya Msaranga Bw Charles Lyimo wakati akizungumzia maendeleo ya shule hiyo baada ya wanafunzi kujiunga na Kidato cha Kwanza kwa mara ya kwanza Januari 9, mwaka huu.

"Shule hii mpya ni ukombozi kwa vijana wa Kata yetu ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu Kwenda kwenye Kata zingine kupata elimu ya Sekondari; iliwabidi kuamka saa 10 za usiku na saa 11 za alfajiri ili waweze kuwahi muda uliowekwa wa kufika shuleni", alisema.

Bw Lyimo alisema uanzishwaji wa shule hiyo pia itawawezesha wanafunzi kufanya vyema kwenye masomo yao kutokana na ukweli kwamba watapata fursa ya kujifunza bila ya kuwa na uchovu ambao walikuwa wanapata kwa kuembea umbali mrefu.

"Hata sisi wazazi tumepata nafuu kubwa maana ilikuwa tunatumia gharama kubwa za usafiri ili waweze kuwahi shuleni haswa msimu wa mvua", alisema.

Bw Lyimo pia alipongeza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kuchangia ujenzi wa Shule hii ya kwanza kabisa katika Kata Msaranga kutokana na fedha za mapato ya ndani za Halmashauri.

"Mchango wa Halmashauri sambamba na ule wa Serikali Kuu umekuja wakati muafaka haswa ikitiliwa maanani ya kuwa Kata yetu haikuwa na shule ya Sekondari kutokana na ile iliyokuweko kupelekwa kata mpya ya Ng'ambo kutokana na mgawanyo uliofanywa na Serikali uliopelekea kuanzishwa kwa kata mpya ya Ng'ambo", alisema.

Akiongelea swala hilo Mkuu wa shule ya sekondari ya Msandaka Bw Erasmus Kyara amesema kuwa ujenzi wa shule hiyo umegharimu jumla ya shilingi milioni 620 kati ya fedha hizo, shilingi milioni 470 zilitolewa na Serikali Kuu na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilichangia jumla ya shilingi milioni 170 kutoka mapato yake ya ndani

Alisema Awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule hii ulihusisha ujenzi wa madarasa nane, meza 160 na viti 160 kwa ajili ya wanafunzi, maktaba, jengo la utawala, jengo la teknolojia ya habari, maabara tatu, vyoo kwa ajili ya wanafunzi na matenki mawili ya maji yenye ujazo wa lita 10,000 kila moja.

Kyara alisema ya kuwa jumla ya wanafunzi 87 walichaguliwa kujiunga na shule hiyo katika kidato cha kwanza kwa mwaka wa 2023 ambapo wanafunzi wasichana walikuwa 51 na wavulana 36. Hadi sasa jumla ya wanafunzi 67 tayari wameanza masomo sawa na asilimia 77 ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule hii.

"Uongozi wa Shule kwa ushirikiano na Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Msaranga unaendelea na taratibu za kuwafuatilia wanafunzi ambao walichaguliwa kujiunga na shule lakini bado hawajaripoti; lengo ni kuhakikisha wale wote waliochaguliwa wanajiunga na elimu ya Sekondari", alisema.

Aidha alisema kuwa uongozi wa shule hiyo unaunga mkono wazo la Halmashauri ya Manispaa ya Moshi la kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi, wazo ambalo alisema litawasaidia wanafunzi kupata muda wa kutosha kujisomea na hivyo kufanya vyema kwenye masomo yao.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo akiwemo Nelvin Lyimo, wameelezea kufurahishwa kwao na ujenzi wa shule hiyo katika Kata hiyo, ambapo wamesema kumewapa ari ya kuendelea na masomo yao.

"Shule hii imetusaidia wanafunzi wa Kata ya Msaranga kupata elimu ya Sekondari karibu zaidi ikilinganishwa na wenzetu waliotutangulia madarasa wakati tukiwa shule ya msingi ambao baada ya kuhitimu Darasa la Saba iliwabidi kusoma shule ambazo iliwalazimu Kwenda umbali mrefu sana kwenda na kurudi kutoka shuleni", alisema.

Naye mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza Maureen Lyatuu alipongeza Serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zilizopelekea kuanzishwa kwa shule hiyo ambayo alisema pamoja na ukaribu wake ina miundombinu yote muhimu ambayo imefanya mazingira rafiki ya kusomea na uhakika kwa wanafunzi na hii itatusaidia kufanya vizuri kwenye masomo yetu.

Kwa upande wake mwanafunzi mwingine Mwanahawa Bakari alisema ujenzi wa shule hiyo ni jambo la kujivunia kwa Kata hiyo kwani haikuwa na shule ya sekondari ya Serikali na kupelekea wanafunzi waliokuwa wanafaulu katika shule za Msingi za Kata hiyo Kwenda kusoma shule zilizipo kwenye Kata nyingine za mbali na kusababisha usumbufu na gharama kubwa za usafiri kwa wanafunzi.

"Hili ni jambo lakujivunia kwa wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba katika Kata hii ya Masaranga kwani kwa sasa watakuwa na uhakika wa kupata elimu ya sekondari karibu zaidi."Alisema

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MIAKA MIWILI

**Mapokezi ya Fedha**

Katika Muda wa Miaka miwili chini ya Uongozi wa Mhe.Dr. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilipokea jumla ya Tsh. **Sh.21,579,937,727.99** kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo na Miradi ya Maendeleo.

| Kifungu | 2021/2022 | 2022/2023 | Jumla |
|---|---|---|---|
| Matumizi mengineyo | 494,088,926.92 | 269,434,000.00 | 763,522,926.92 |
| Miradi ya Maendeleo | 6,444,754,652.87 | 3,125,604512.66 | 9,570,359,165.53 |
| Mapato ya ndani | 6,315,890,892.32 | 4,930,164,743.22 | 11,246,055,635.54 |
| **Jumla** | **13,254,734,472.11** | **8,325,203,255.88** | **21,579,937,727.99** |

Kati ya Fedha hizi, **Tsh. 9,570,359,165.53** zimetumika kutekeleza miradi kama ifuatavyo:

**Miradi iliyotekelezwa Mwaka 2021/2022**

| NA | JINA LA MRADI | GHARAMA |
|---|---|---|
| 2.2.1 | **Fedha za Mapato ya ndani** | |
| 1 | Ujenzi wa madarasa 13 katika Shule za Msingi Mandela(1),Chemchem(1),Msaranga(2),Shirimatunda(1), Mnazi (2),Azimio(1),Langoni(3) na Njoro(2) | 260,000,000.00 |
| 2 | Ujenzi wa madarasa matatu(3) katika Shule ya Sekondari Anna mkapa | 60,000,000.00 |
| 3 | Ukarabati/Umaliziaji wa madarasa 18 katika Shule za Sekondari Mji mpya(6),Msasani(6), na Regnald Mengi (6). | 90,000,000.00 |
| 4 | Ujenzi wa matundu 62 ya Vyoo katika Shule za Msingi Uhuru(8), Langoni(8),Magereza (14), Mawenzi(8),Moshi (4),Mwenge(8),Rau(4) na Shaurimoyo(8) | 140,000,000.00 |
| 5 | Ukarabati/Ukamilishaji wa ujenzi wa maabara ya fizikia katika shule ya sekondari Msasani. | 16,000,000.00 |
| 6 | Ununuzi wa vitanda bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Karanga | 22,000,000.00 |
| 7 | Ujenzi wa vyoo matundu 4 katika zahanati ya Njoro | 10,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Ukarabati wa Soko la pasua | 50,175,327.28 |
| 9 | Ujenzi wa vyoo matundu 12 katika soko la Memorial | 45,000,000.00 |
| 10 | Ukarabati wa nyumba 5 za watumishi | 7,241,050.00 |
| 11 | Matengenezo ya taa za barabarani | 7,000,000.00 |
| 12 | Kuendeleza Ujenzi wa stendi ya Ngangamfumuni | 270,000,000.00 |
| 13 | Ukarabati wa ofisi kuu Halmashauri | 4,036,575.00 |
| 14 | Uwekaji wa postikodi za makazi | 10,000,000.00 |
| 15 | Ujenzi wa uzio katika machinjio Kiborloni | 15,000,000.00 |
| 16 | Ukamilishaji wa ghala la kuhifadhia mpunga katika kata ya Kaloleni | 20,000,000.00 |
| 17 | Utoaji wa mikopo kwa vikundi | 949,398,700.00 |
| | **Jumla** | **1,975,851,652.28** |
| 2.2.2 | **Fedha za Mfuko wa Jimbo** | |
| 1 | Ukarabati wa kituo cha polisi kata ya Kaloleni | 5,700,000.00 |
| 2 | Kupaka Rangi nyumba ya Mwalimu SM msaranga | 1,500,000.00 |
| 3 | Ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi ya Mtaa wa Matindigani | 3,000,000.00 |
| 4 | Kujenga Kivuko kinachounganisha mtaa wa Mjimwema kwenda Njoro | 3,000,000.00 |
| 5 | Ukarabati wa stoo katika shule ya sekondari korongoni | 1,200,000.00 |
| 6 | Ununuzi wa samani katika Ofisi ya kata ya Soweto | 1,800,000.00 |
| 7 | Ununuzi wa samani kata ya Njoro | 3,000,000.00 |
| 8 | Ujenzi wa Calvat katika barabara ya Yehova Mtaa wa Sokoni | 3,000,000.00 |
| 9 | Ukamilishaji wa matundu ya vyoo ya vyoo katika Ofisi ya Kata Ng'ambo(2),Shule za msingi J.K.Nyerere(3)Shaurimoyo(18), Zahanati ya Rau (2) na Shule ya Sekondari Kiusa(12) | 13,487,350.00 |
| 10 | Ukarabati wa madarasa 4 katika shule ya msingi Moshi | 3,000,000.00 |
| 11 | Utengenezaji wa madawati 27 shule ya msingi Mandela | 471,650.00 |
| 12 | **Jumla** | **39,159,000.00** |
| 13 | **Fedha za Serikali kuu** | |
| 14 | Ujenzi wa vyumba 22 vya madarasa katika shule za sekondari 10 | 440,000,000.00 |
| 15 | Ujenzi wa miundombinu za kunawia mikono katika shule za msingi Kaloleni na Jitegemee | 23,744,758.00 |
| 16 | Ujenzi wa vyoo matundu 18 ya wanafunzi katika shule za msingi Azimio (6),Mandela (6) na Shirimatunda 6 | 19,800,000.00 |
| 17 | Ujenzi wa miundombinu ya kunawa mikono katika shule ya sekondari Mji mpya | 11,872,379.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Ujenzi wa kituo cha afya Shirimatunda | 500,000,000.00 |
| 19 | Ujenzi wa Sekondari mpya ya Msandaka kata ya Msaranga | 470,000,000.00 |
| 20 | Ujenzi wa hospitali ya wilaya | 500,000,000.00 |
| 21 | Ujenzi wa jengo la Ofisi Kuu | 1,000,000,000.00 |
| | **Jumla** | **2,965,417,137.00** |
| | **JUMLA KUU MIRADI 2021/2022** | **4,980,427,789.28** |

**Miradi iliyotekelezwa Mwaka 2022/2023 hadi March, 2023**

| NA | JINA LA MRADI | GHARAMA |
|---|---|---|
| **2.3.1** | **Fedha za Mfuko wa Jimbo** | |
| 1 | Kukarabati Calvat la Barabara ya Msikitini | 3,000,000.00 |
| 2 | Umaliziaji wa jengo la Dhobi la kufulia Zahanati ya kata ya Longuo "B" | 1,500,000.00 |
| 3 | Ununuzi wa Samani za Ofisi ya Kata,Ambazo ni meza 6, viti 6, panga boy (ceiling fan) 4, na kabati za kutunzia kumbukumbu za ofisi na file 3. | 5,000,000.00 |
| 4 | Ukarabati wa skip backet | . 3,000,000.00 |
| 5 | Uwekaji wa taa za solar katika masoko ya manyema, mbuyuni na soko la kati | 4,800,000.00 |
| 6 | Ukamilishaji wa ujenzi wa matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Tumaini | 3,000,000.00 |
| 7 | Umaliziaji wa Choo Zahanati Rau | 1,700,000.00 |
| 8 | Samani za Ofisi | 3,000,000.00 |
| 9 | Ununuzi wa samani za kituo cha polisi | 4,999,000.00 |
| 10 | Ukarabati mdogo wa Shule ya Msingi Mnazi | 2,997,000.00 |
| 11 | Utengenezaji wa milango 4 (milango 3 ya choo na mlango 1 wa mbele) Ofisi ya Kata | 1,000,000.00 |
| 12 | Matofali 2000, kwa ajili ya ofisi ya Kata na Kituo cha Polisi | 3,000,000.00 |
| 13 | Kukamilisha darasa lilijengwa na lions club | 8,000,000.00 |
| 14 | Kukamilisha ujenzi wa choo Ofisi ya Kata | 1,028,000.00 |
| 15 | Kumalizia mfereji ulioko ndani ya kivuko Mtaa wa Sokoni | 1,500,000.00 |
| 16 | Ujenzi wa Ofisi ya kata (ununuzi wa mchanga na mawe) | 3,000,000.00 |
| 17 | Ununuzi wa pikipiki 2 za polisi(TVS) | 6,000,000.00 |
| 18 | ununuzi wa magodoro 5 , blanketi na mashuka 5 katika idara ya zimamoto na uokozi | 1,000,000.00 |
| 19 | Kivuko kinachounganisha mtaa wa sokoni kata ya njoro na Arabica kata ya miembeni (BI USI) | 5,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **62,524,000.00** |

**FEDHA ZA MAPATO YA NDANI**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kujenga matundu ya vyoo 125 katika Shule za msingi (Chemchem 12,Jitegemee 12,Korongoni 3, Majengo 10,Miembeni 12, Njoro 10, Rau 10, Shaurimoyo 18, Sokoine 8, Kaloleni 12 na Soweto 8) | 113,000,000.00 |
| 2 | Ujenzi wa uzio wa Ukuta katika shule za Msingi Kaloleni na Sekondari ya Mji Mpya | 60,000,000.00 |
| 3 | Ujenzi/ Ukarabati wa madarasa 11 katika Shule za Msingi (Karanga 1, Kilimanjaro 1,Langoni 2, Mnazi 1,Uhuru 1 na Sekondari ya Mji Mpya 5) | 141,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Kukamilisha ujenzi wa nyumba za mwalimu Shule za Msingi (Karanga , Mandela,Moshi) na Sekondari (Msaranga na karanga) | 128,000,000.00 |
| 5 | Ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya ya Msandaka | 150,000,000.00 |
| 6 | Kukarabati miundombinu ya Zahanati ya Kaloleni | 20,000,000.00 |
| 7 | Upanuzi Zahanati ya Msandaka kuuwa Kituo cha Afya | 330,000,000.00 |
| 8 | Kujenga eneo la kufulia kwenye Kituo cha Afya cha Pasua | 9,000,000.00 |
| 9 | Kujenga kichomea taka kwenye Zahanati ya Shirimatunda | 25,000,000.00 |
| 10 | Kuwezesha matengenezo ya barabara za Kata | 55,452,000.00 |
| 11 | Kuendeleza Ujenzi wa Uwanja wa Majengo | 300,000,000.00 |
| 12 | Kuwezesha Ukarabati wa Ofisi kuu za Halmashauri | 6,039,300.00 |
| 13 | Ujenzi wa Kibanda cha walinzi katika dampo la Mtakuja | 10,000,000.00 |
| 14 | Ukarabati machinjio 2-Kiborloni na Bondeni | 15,000,000.00 |
| 15 | Matengenezo wa masoko 4 kwa kumwaga changarawe | 20,271,250.00 |
| 16 | Ukarabati soko la Majengo | 60,000,000.00 |
| 17 | Ujenzi wa vivuko na vyoo eneo la machinjio kuu | 50,000,000.00 |
| 18 | Utoaji wa Mikopo kwa Vikundi vya wanawake | 64,394,641.00 |
| 18 | Kufunga mfumo wa CCTV Camera jengo la utawala | 30,000,000.00 |
| 20 | Ukamilishaji wa Ofisi ya Kata Mfumuni | 10,000,000.00 |
| 21 | Ukarabati ofisi ya Mtaa wa Kanisani | 8,242,299.12 |
| 22 | Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Mawenzi | 50,000,000.00 |
| 23 | Ununuzi wa maghuba mawili (2) ya kukusanyia taka ngumu | 30,000,000.00 |
| | **Jumla** | **1,685,399,490.12** |
| **2.3.3** | **Fedha kutoka Serikali Kuu** | |
| | Ujenzi wa madarasa 10 na madawati | 200,000,000.00 |
| | **Jumla** | 200,000,000.00 |
| | **JUMLA KUU MIRADI 2022/2023 HADI MARCH,2023** | **1,947,923,490.12** |

# UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Utoaji wa mikopo kwa 10% ya Mapato ya ndani kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu**

Katika kipindi cha miaka Miwili Serikali imetoa Mikopo kwa Vikundi 284 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu jumla ya Tsh. 1,682,778,990.00 kwa mchanganuo ufuatao:

| Mwaka | Jumla ya Kiasi Kilichotolewa | Jumla ya Vikundi vilivyopata Mkopo | Mchanganuo wa Idadi ya vikundi na kiasi kilichotolewa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Vijana | | Watu wenye Ulemavu | |
| | | | Kiasi | Idadi | Kiasi | Idadi | Kiasi | Idadi |
| 2021/2022 | 949,398,700.00 | 159 | 667,343,700 | 116 | 256,555,000 | 32 | 25,500,000 | 11 |
| 2022/2023 | 733,380,290.00 | 125 | 479,380,102 | 88 | 230,309,188 | 29 | 23,500,000 | 8 |
| **Jumla** | **1,682,778,990** | **284** | **1,146,723,802** | **204** | **486,864,188** | **61** | **49,000,000** | **19** |

## Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini [1]

Kwa Muda wa miaka miwili Serikali kupitia Mfuko wa kunusuru Kaya Maskini (TASAF) umehawilisha fedha kiasi cha Sh. 708,391,040.31 kwa kaya maskini 1,666 ndani ya kwenye Mitaa 59 ya Manispaa.

# TASAF YAENDELEA KUBADILISHA MAISHA YA WAKAZI WA MANISPAA



Mary Paulo (43), ni mkazi wa Kata ya Kilimanjaro ni mama wa watoto watatu, ambaye ni mnufaika wa mradi wa TASAF.

"Mimi Kabla ya kujiunga Na mpango wa TASAF Maisha yalikuwa magumu, nilikuwa sina mtaji wa kufanya biashara, nilishindwa kuwalipia watoto mahitaji muhimu ya shule na kupelekea hata kushindwa kumudu garama za chakula"anasema Mary Paulo.

Ni kauli ya Mary ambaye anapokea kiasi cha Tsh 46,000 ambayo imemuwezesha kuwasomesha watoto wake, mmoja akiwa anasoma elimu ya chuo, mwingine alimu ya sekondari, na wa mwisho akisoma elimu ya msingi.

Anasema baada ya kujiunga na Tasaf maisha yamebadilika kwa kuweza kulipa ada za watoto shuleni, pamoja na kuanza kufuga kuku ambapo mtaji umekua hadi kuanza mradi wa kuuza nguo.
"Nilianza na vifaranga 50 kwa tsh 100,000 fedha ambayo niliipata baada kuweka fedha kidogo kidogo na baada ya kuuza kuku pia nilipa mtaji na kuanza kununua nguo na kutembeza"
Mara ya kwanza nlikuwa sijapata ushauri wa wataalamu hivyo vifaranga nilivyonunua vilikufa ikabili kukusanya fedha kidogo kidogo hadi nilipokuwa na tsh 280,000 na kununua kuku wakubwa 40 kwa tsh 7000 kila mmoja ambao waliniwezesha nikauza mayai na kuku wenyewe na kisha nikanunua tena vifaraga 100.

"Ufugaji umenisaidia kulipa ada za watoto shule,pamoja na kujiunga kwenye vikundi, hali iliyoniwezesha kuanza mradi wa nguo na mtaji wa Tsh 300,000, na mpaka sasa mtaji wangu umekua na kufika tsh 600,000, hivyo nawashauri wanufaika wengine kufanya mradi kuku kwani umekuwa na mchango mkubwa kwenye maisha yangu"Anasimulia ..




# BAJETI YA 2023 / 2024

Baraza la Madiwani la Manispaa ya Moshi kwa kauli moja limepitisha mpango na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024 kwa jumla ya Tshs 50,639,993,000

Mstahiki Meya wa Manispaa Mhandisi Zuberi Kidumo, alitangaza bajeti hiyo , wakati akifunga kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi kujadili na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti na kueleaza kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Shs 8,091,260,000, Matumizi ya kawaida (OC) ni Shs 743,409,000, Miradi ya Maendeleo ni Shs 9,792,485,000 na kwa upande wa Mishahara
inatarajiwa kuwa Shs 32,012,839,000 hivyo kufanya jumla ya Bajeti ya Manispaa ya Moshi kuwa Shs .50,639,993,000.

"Manispaa ya Moshi inahikikisha kuwa inatekeleza ila ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 na imejipanga kuweka nguvu zake zaidi katika ukusanyaji mapato na kusimamia miradi miradi ya maendeleo ili kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa wananchi na wakazi wa Manispaa ya Moshi"alisema Mhandisi Zuberi



# MIAKA MIWILI YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA INAYOONGOZWA NA MHE.DR. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## MIKOPO ISIYO NA RIBA

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kipindi cha Miaka miwili imefanikiwa kutoa mikopo isiyo na riba yenye Jumla Tshs. 1,682,778,990 kwa vikundi 284 ikiwa ni utekeleza wa agizo la serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa Dr Samia Suluhu Hassan la kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Wanawake,Vijana na Watu Wenye Walemavu.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii Bi. Rose Minja ameeleza kuwa mikopo hiyo imetolewa kwa vikundi vya wajasiriamali mbalimbali kwenye Kata 21 za Manispaa ya Moshi ambapo Vikundi 204 vya wanawake vimepata Shs 1,464,723,802 vikundi 61 vya vijana vimepewa Ths 486,864,188 na vikundi 11 vya Watu Wenye Ulemavu vimepata kiasi cha Ths 49,000,000.

"Kumekuwepo na mwitikio mkubwa kwa makundi yote ukiacha kundi moja la Watu Wenye Ulemavu,ambapo tumekuwa tukisisitiza kujikita katika kuanzisha miradi yenye tija ili kuweza kupata matokeo chanya kwenye uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa" Alisema Bi Rose Minja

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana Haque Scale Manufacturer kinachojishughulisha na utengenezeji wa mizani Bw. Hatibu Hamidu ameeleza kuwa kikundi chao tayari kimenufaika katika awamu mbili, awamu ya kwanza wakipatiwa mkopo wa Tsh Milioni 5 na awamu ya pili walipatiwa Tsh 8,000,000 Wamekiri kuwa mkopo huo umewawezesha kununua vitendea kazi na malighafi na kwa sasa wanaweza kuendesha maisha yao ya kila siku na kuweza kuzihudumia familia zao.

"Mikopo tuliyopewa imetusaidia kutoka sehemu moja kwenda nyingine, ukiangalia maisha ya hapo nyuma kabla ya kupata hii mikopo yalikua magumu kwavile mtaji wetu ulikua mdogo sana, hivi sasa tunaweza kuendesha biashara yetu na tunajikimu kwenye mambo mengine " alisema Bw. Hatibu Hamidu

Tunaishukuru Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kutunga sheria inayowajali na iliyoboresha utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwani kikundi chetu kimeweza kunufaika na mkopo huu usio na riba.

# TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI ANAWATANGAZIA WAFANYABIASHARA WOTE NA TAASISI ZOTE KUWA UTOAJI NA ULIPAJI WA LESENI ZA BIASHARA, VILEO, HOTEL LEVY NA KODI YA HUDUMA (SERVICE LEVY) ZINATOLEWA AU KULIPWA KWA KUTUMIA MFUMO MPYA WA TAUSI.

MFUMO HUU MPYA UNAMUONDOLEA MFANYABIASHARA USUMBUFU WA KWENDA OFISI ZA BIASHARA AU OFISI YA MAPATO KWA AJILI YA ULIPAJI/UKATAJI WA LESENI KWANI UNAWEZA KUPATA HUDUMA HIZO KWA KUTUMIA SIMU YAKO (SIMU JANJA).

KWA SASA MFANYABIASHARA UTAINGIA KWENYE MFUMO WA TAUSI KUPITIA SIMU YAKO JANJA NA KUFANYA MAOMBI YA LESENI YAKO. NI RAHISI KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA TAUSI:-

(I) UNAPASWA KUWA NA NAMBA YA NIDA PAMOJA NA NAMBA YAKO ILIYOTUMIKA KUSAJILI NIDA.

(II) INGIA KWENYE APPLICATION GOOGLE HALAFU ANDIKA tausi.tamisemi.go.tz HALAFU BOFYA CREATE ACCOUNT KISHA FUATA MAELEZO ILI KUJISAJILI.

ILI KUOMBA LESENI YA BIASHARA MFANYABIASHARA UTAWASILISHA MAOMBI YA BIASHARA YAKO KUPITIA SIMU YAKO KATIKA MFUMO HUU MPYA WA TAUSI.

HAKIKISHA UNAAMBATISHA VITU MUHIMU VIFUATAVYO WAKATI WA KUOMBA LESENI:-

(a) TAX CLEARENCE CERTIFICATE YA SASA.
(b) MKATABA WA PANGO.

BAADA YA KUKAMILISHA MAOMBI AFISA BIASHARA ATAYAPITIA NA KURUHUSU UWEZE KUJITENGENEZEA LESENI YAKO YA BIASHARA AMBAYO NI YA DIGITAL BAADA YA KULIPIA KWA CONTROL NAMBA AMBAYO UTAIPATA KUPITIA SIMU YAKO.

**NB:** KWA MAELEZO NA UFAFANUZI ZAIDI FIKA OFISI YA BIASHARA CHUMBA NA. 24 AU PIGA SIMU ZIFUATAZO: 0713-902492, 0753-019427, & 0754-860670.

**IMETOLEWA NA:**

Rashid K. Gembe
**MKURUGENZI**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI



## MANUFAA YA KUTUMIA MASHINE ZA KIELECTRONIC KUKUSANYIA MAPATO(POS)

- Kwa Kutumia POS Ni Rahisi Kupata Taarifa Za Makusanyo
- Uhakika Wa Fedha Zote Zinazotozwa Kuingia Halmashauri
- Kudhibiti Wizi Wa Fedha Zinazotozwa

*Dai Risiti Kulingana Na Kiasi Cha Pesa Ulichotoa*

moshimanispaa www.moshimc.go.tz

TANZANIA

# MANISPAA YETU

www.moshimc.go.tz | Toleo La 02 | Kitengo cha Mawasiliano | Manispaa ya Moshi

